# 14. JAMAA YA ISRAELI KATIKA MISRI

**“Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha yenu kwa wokovu mkuu”**

**Shabaha**

Kuonyesha jinsi Mungu alivyofanya kazi kupitia Yusufu katika Misri ili kuwaoka wana wa Israeli, familia ya Yakobo.Yusufu aliwatuma ndugu zake wakiwa na chakula lakini pia alikuwa anawapima. Kwa siri akarejesha fedha zao katika magunia yao, akamweka Simeoni kifungoni na akadai wamlete amwone Benyamini.Yakobo asingemruhusu Benyamini aondoke, lakini mwishowe chakula kiliisha na hiyo iliwabidi warudi tena Misri.Habari hii inaishia katika furaha wakati Yusufu anapojitambulisha kwa ndugu zake na kwa baba yake,mzee Yakobo anakwenda kwake katika Misri.

Mwanzo 43 – 50

## NDUGU ZAKE YUSUFU WANAKWENDA MISRI MARA YA PILI:Mwanzo 43 na 44

Alikuwa ni Yuda ambaye mwishowe alimshawishi Yakobo kumruhusu Benyamini kwenda pamoja nao, akiahidi kurudi naye nyumbani akiwa salama. Walichukua zawadi kwa mtawala na fedha mara mbili ya zile za awali katika magunia yao na Yakobo akaomba:**“Mungu mwenyezi na awape rehema usoni pa mtu yule”** (Mwanzo 43:14)

Walipowasili walipelekwa nyumbani kwa Yusufu ambako tafrija iliandaliwa kwa ajili yao.Yusufu aliwakaribisha kwa kuwapanga katika meza kwa kufuata umri wao na jambo liliwashangaza. Mwoshowe Benyamini alipewa chakula chake mara tano ya wengine na walikifurahia chakula wakiwa wanakula pamoja naye. Kisha wakiwa na magunia yao yaliyojazwa nafaka walianza safari ya kurudi nyumbani wakiwa pia na Simeoni ambaye alikwisha rejeshwa kwao na Benyamini halikadhalika akiwa salama. Hata hivyohawakuweza kufika mbali kabla mjumbe wa Misri kuwashika kwa kuwatuhumu kuiba kikombe cha fedha cha bwana wake, ndugu hao walikana mara moja, ikiwa mmoja wao atakuwa na kikombe cha fedha inampasa kufa.Lakini upekuzi ulipofanywa, kikombe cha fedha kilikutwa katika mfuko wa Benyamini!Kwa haraka mara moja walirejea tena Misri kuomba msamaha na Yuda aliomba kuadhibiwa badala yake,kwa maana alikuwa amemwahidi baba yake kuwa atamrudisha Benyamini nyumbani akiwa salama.

## YUSUFU NA NDUGUZE KATIKA MUUNGANO WA FURAHA :Mwanzo 45

Wakati sasa ulikuwa umefika kwa Yusufu kuwaambia ndugu zake kuwa yeye alikuwa nani. Hivyo waliondoa watumishi nje ya chumba na kulia kwa sauti “**Mimi ndimi Yusufu,baba yangu angali hai?”** (mstari 3).Waliogopa sana,wakikumbuka yote waliyomtendea, lakini aliwaambia wasiwe na wasiwasi: **“Basi sasa msihuzunike wala msifadhaike katika nafsi zenu kwa kuniuza huku,maana Mungu alinipeleka mbele yenu…kuhifadhi maisha yenu kwa wakovu mkuu”** (mistari 5,7).Akawaambia wakurudi Kanaani na kumleta Yakobo baba yake naye katika Misri, pamoja na familia yote na mifugo na vitu vyao.Na kuwa atawapatia sehemu ya nchi ya Misri iliyoitwa nchi ya Gosheni ili kuishi huko na kuwatunza mpaka njaa itakapokwisha.

Aliwafungashia zawadi za nguo,nafaka,mikate na nyama na magari ya kubeba na kuleta familia yao katika Misri.Kwa hiyo ndugu zake waliharakisha kurudi nyumbani kwa baba yao wakiwa na habari za kufurahisha na kustaajabisha**-“Yusufu yu ngali hai na ni mtawala katika nchi yote ya Misri”** (mstari 26)

likuwa vigumu kwa Yakobo kuwaamini, lakini baada ya kusikia masimulizi yao na kuona magari na akajawa na furaha.Akashukuru akawapokea wanawe na kujiandaa kuondoka kuelekea kwenye nchi ya neema kuwa pamoja na Yusufu katika Misri: **“Yatosha Yusufu mwanangu angali hai,nitakwenda nionane naye kabla sijafa”** (Mwanzo 45:28)

## YUSUFU ANAKWENDA KUMLAKI YAKOBO:Mwanzo 46:28-30

Akiwa njiani kuelekea Misri,Yakobo alisimama Beer-sheba na huko akamtolea Mungu dhabihu akimshukuru kwa wema wake. Mungu alizungumza na Yakobo usiku katika maono, akasema **Mimi ni Mungu, Mungu wa baba zako usiogope kushuka mpaka Misri maana nitakufanya taifa kubwa** (Mwanzo46:3 – 4) Kisha Yakobo akaondoka alfajiri na kuendelea kwenda Misri akiongozana na wanawe pamoja na familia zao.

Yusufu alipanda gari lake kuelekea nchi ya Gosheni, ambako furaha ya kukutana kati ya baba na mwanawe ilifanyika (mstari 29).Yusufu alikaribisha familia yake katika Misri na Yakobo ambaye alidhani hatamwona tena mtoto wake mpendwa, mwishowe alifurahi kwa hakika alihisi wema a Mungu kwa kuwa sala yake ilijibiwa.Alionyesha mawazo yake katika maneno haya **“Na nife sasa kwa kuwa nimekuona uso wako ya kuwa ungali hai”** (Mwanzo 46:30)

## WAEBRANIA WANAHAMIA KATIKA NCHI YA GOSHENI –WANAJITENGA NA WAMISRI Mwanzo 47:1 – 10

Yusufu aliwapeleka ndugu zake watano mbele ya Farao,akawasisitiza wamwambie kwamba walikuwa wachungaji na wamwombe kama inawezekana waishi katika nchi ya Gosheni. Nchi hii ilikuwa ni eneo zuri kwa kuchungia mifugo na lilijitenga kutoka katika eneo lote la Misri.

Farao alikubali na hata kuwaweka kuwa waangalizi wa mifugo yake. Nchi ya Gosheni ilikuwa upande wa mashariki ya mto wa Naili, na ilikuwa imezungukwa na milima kila upande, kwa hiyo Waisraeli walikuwa wamejitenga na Wamisri-somo ambalo inatupasa kujifunza, kujitenga na dunia na sio kujifunza njia zake.Yusufu alimtambulisha baba yake kwa Farao na Yakobo alimbariki Farao na kumweleza maisha yake katika Kanaani na kwamba alikuwa na umri wa miaka 130.

## YAKOBO ANAFARIKI:Mwanzo 47:28 – 31

Miaka kumi na saba ilipita na Yakobo alikuwa na umri wa miaka 147 na wakati ulifika wa yeye kufariki. Alimwita kwake Yusufu na kumtaka aahidi kutomzika Misri, bali kumbeba kumtoa nje ya Misri na kumzika katika eneo la mazishi la Abrahamu na Isaka katika nchi ya Kanaani. Baada ya kuwabariki wanawe wote, alifariki na Yusufu alitimiza ahadi yake na kumzika baba yake katika nchi ya Kanaani.

## KIFO CHA YUSUFU :Mwanzo 50: 23 – 26

Yusufu aliendelea kuishi Misri mpaka watoto wa watoto wake walipozaliwa. Alipokaribia kufa alitoa ujumbe wa mwisho kwa wana wa Israeli, akawakumbusha kwamba Mungu angewatoa kutoka Misri kwenda tena katika nchi ya Kanaani! **"Mungu atawajia ninyi bila shaka, atawapandisha kutoka nchi hii mpaka nchi aliyowaapia, Ibrahimu na Isaka na Yakobo"** (Mwanzo 50:24). Akawafanya waahidi kupeleka mifupa yake kwa mazishi watakapokuwa wakirudi katika nchi ya ahadi.Yusufu alikuwa na umri wa miaka 110.

## FUNDISHO KWETU SISI

Ingawa Yusufu aliishi Misri kamwe hakupoteza mwelekeo wake wa Tumaini la Israeli.

Alijua kwamba siku itakuja ambayo wataiacha nyuma Misri na kuondoka, kwa hiyo alionyesha imani yake kwa kuomba waipeleke mifupa yake wakati watakapoondoka Misri.

Sisi nasi,kama Yusufu pia inatupasa kutosahau,kwa kuwa maisha yetu ya baadaye yanategemea Ufalme wa Mungu,na kamwe tusijihusishe katika mambo ya dunia yanayotuzunguka, isipokuwa tuwe tayari kuyaacha nyuma yote wakati Bwana Yesu atakapokuja. Inatupasa kuonyesha imani sawa na ya Yusufu, tukiamini kwa ukamilifu kwamba yote Mungu aliyoahidi atayafanya.

Pia zingatia,kwamba ingawa nchi ya Kanaani iliahidiwa kwa Yakobo, alikufa katika nchi ya Misri bila ya kupokea urithi wake.Hii inaonyesha kwamba ahadi hizo hazijatimizwa.Yakobo ni lazima afufuliwe kutoka kwa wafu ili kwamba ahadi itimizwe.Na hili ndiyo tumaini la mababa (Matendo ya Mitume 26:6)

Mara hii tena, matukio haya tuliyoyafikiria ni aina ya matukio yanayohusiana na maisha ya Bwana Yesu Kristo.Katika sura hizi zia mwisho tunakumbushwa juu ya mambo ambayo yatatokea atakaporudi kama mfalme na kujitambulisha kwa watu wake,Wayahudi

| | |
|---|---|
| 1. Ndugu zake hawakumtambua (Mwanzo 42.8) | Wayahudi hawatamtambua Yesu kuwa ni nani atakaporudi(Zekaria 13:6) |
| 2. Yusufu alijitambusha kwa nduguze (Mwanzo 20:45.1) | Yesu atajidhirisha mwenyewe kwa wayahudi (Zekaria12:10) |
| 3. Waliingiwa na hofu mbele yake (Mwanzo 45:3) | Nao wataomboleza (Zekaria 12:10) |
| 4.Yusufu alisema kuwa Mungu alimpeleka kuyahifadhi maisha yao | Yesu ataleta wokovu na Wayahudi watamgeukia Mungu (Warumi 12:26) |
| 5. Yusufu alitawala na kumiliki mali ya ulimwengu ya (Mwanzo 47;14) | Yesu atamiliki utajiri wa mataifa (Isaya 60: 11 – 12) |
| 6. Yusufu alinunua ardhi yote kwa ajili ya Farao (Mwanzo 47:20) | Yesu atatawala hadi miisho ya dunia (Zab. 72) |

## MASWALI

1. Nani aliyeahidi kumlinda Benyamini?
2. Ni jinsi gani Yusufu aliwaketisha ndugu zake katika meza?
3. Kiasi gani cha chakula Yusufu alimpatia Benyamini?

4. Kikombe cha fedha kilipatikana katika kikapu cha nani ?
5. Je Yusufu alisema nini wakati alipojitambulisha kwa ndugu zake?
6. Je Yusufu aliwachukia ndugu zake?
7. Familia ya Yakobo ilikwenda kuishi wapi ?
8. Yakobo alipofariki alizikwa wapi i?
9. Wosia wa Yusufu kuhusu mifupa yake ulikuwa upi?

### Majibu ya Kina

1. Yusufu alikuwa tajiri na mtu maarufu katika Misri

a. Nini kilitokea kwa ndugu zake katika safari ya pili ya kununua nafaka?
b. Kwa nini Yusufu aliwasamehe ndugu zake?

2. Yusufu aliwatuma ndugu zake kumleta baba yao na familia zao katika Misri.

a. Ni wapi wana wa Israeli kuishi katika Misri?
b. Ni kwa nini sehemu hii ilikuwa nzuri?
c. Tunapata fundisho gani katika somo hili?

3. Ni upi ulikuwa wosia wa mwisho wa Yusufu kwa watu wake kabla ya kufariki

### Majibu ya Nyongeza

Tayari tumeona kwamba Yusufu alikuwa ni kivuli cha Kristo (angalia somo la 12) onyesha jinsi matukio ya habari hii yanavyoelekeza ujio wa pili wa Kristo (orodhesha matukio mengi kadri uwezavyo).